

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



Agosti 28, 2022

**WILAYA YA LUDEWA YAKAMILISHA ZOEZI LA SENA KWA DODOSO KUU KWA
ZAIDI YA ASILIMIA MIAMOJA**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere amewashukuru wananchi wa Wilaya ya Ludewa kwa mwitikio mkubwa walioutoa katika zoezi la Sena ya watu na Makazi lililoanza Agosti 23, 2022.

Katika zoezi hilo Kaya zaidi ya 38,000 zimehesabiwa mpaka kufikia leo Agosti 28, 2022 ambapo matarajio ya zoezi hili kabla ya kuanza kutekelezwa ilikadiliwa kuzifikia kaya 35,730.00 ambapo kukamilika kwa zoezi hili leo limeifanya Wilaya ya Ludewa kupita lengo lililokuwa limekadiliwa na sasa zoezi hilo limekamiliwa kwa kuzifikia kaya zote za Wilaya ya Ludewa zenyejumla ya Kaya 38,523.00 kwa kata 26.

Akizungumza mara baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Mratibu wa zoezi hilo ya namna zoezi lilivyofanyika katika Wilaya ya Ludewa amesema kuwa, kazi kubwa iliyofanywa na wananchi, makarani, viongozi wa vitongoji na vijiji pamoja na kamati ya Sena ya Wilaya inapaswa kupongezwa kwa kuhakikisha wananchi wote wamehesabiwa.

Mratibu wa Sena Wilaya ya Ludewa Bwn. Alex Henjewele akitoa taarifa ya zoezi hilo amesema mpaka kufikia leo Jumapili Agosti 28, 2022 jumla ya Kaya 38,523.00 tayari zimehesabiwa ambapo ni zaidi ya asilimia 100.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Sena ya Wilaya ya Ludewa amesema ushirikiano mkubwa uliopo baina ya wananchi, makarani, viongozi wa vijiji na Kamati zote za Sena umefanya kazi iwe rahisi na kufikia asilimia zaidi ya 100 katika kazi hiyo.

A handwritten signature in blue ink.

Chrispin B. Kalinga
Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini
Halmashauri (W) Ludewa.